KATIBA KUU YA FAMILIA YA WASALVATORIANI

UTANGULIZI

Usithubutu kupumzika hata kwa nukta moja kama
Kuna binadamu mmoja katika dunia
Ambaye hamjui Mungu
Na hampendi Mungu zaidi ya vitu vyote.

Usithubutu kupumzika hata kwa nukta moja
Mpaka Mungu anasifiwa popote.

Usithubutu kupumzika hata kwa nukta moja
Mpaka Malkia wa mbingu na dunia anasifiwa popote.

Kwa msaada wa neema ya Mungu,
Sadaka yoyote ile, hata Msalaba, upweke, jaribio, kishawishi
Na hata kitu kingine chochote havitakuwa vigumu mno kwako.
Ninaweza kufanya kila kitu katika Mungu anayeniimarisha.

Jaribio lolote lile, hata ukafiri, ulegevu na hata dhuluma yoyote ile
Visipunguze jitihada yako ya kitume!

Lakini kila kitu kwa njia ya Mungu, pamoja na Mungu na kwa ajili ya Mungu.
Watu wote, makabila yote na mataifa na lugha zote
Wamsifu Bwana, Mungu wetu.

Ole wangu, Bwana wangu
Kama sitakutangaza kwa wanaume na wanawake

Ee Bwana unisaidie na unionyeshe njia!
Bila wewe siwezi kufanya chochote.
Ninatumainia kila kitu toka kwako.
Katika wewe Bwana nimekuwa ninatumaini,
Na sitaaibishwa kamwe.

Sali muda wote katika unyenyekevu wa ndani
Na katika matumaini makubwa kabisa.
Usikubali chochote kikuzuie kufanya hivyo.

Padre Fransis Maria wa Msalaba Jordani
Shajara ya Maisha ya Kiroho II, 1-2
Tarehe 20 Desemba, 1894.

MOJA
WITO WETU NA KARAMA YETU

"Na *uzima wa milele ndiyo huu: Kukujua wewe uliye peke yako Mungu wa kweli, na Yesu Kristu uliyemtuma."*
Yohana 17:3

1. Akivutwa na mang'amzi ya ndani juu ya Mungu na hali ya Kanisa la wakati wake, Padre Fransis Maria wa Msalaba Jordan alikuwa na tamaa kubwa sana kwamba watu wote wamjue Mungu mmoja wa kweli na wapate mang'amzi ya utimilifu wa uzima kwa njia ya Yesu Mwokozi. Nia yake ilikuwa kuunganisha nguvu zote za kitume katika Kanisa kumpenda na kumtangaza Yesu kama Mwokozi katika ulimwengu unaomhitaji Mungu. Aliwahusisha watu wa rika na hali zote za maisha, ili kufanya kazi pamoja kila mahali na kwa njia yoyote na namna zozote.

2. Familia ya Kisalvatoriani ni mwonyesho wa karama, zawadi ya Roho Mtakatifu aleyepewa Padre Jordani kwa ajili ya Kanisa. Tunafuata asili yetu kwenye Shirika Fundishi la Kitume, lililoanzishwa na Padre Jordani Tarehe 8 Desemba 1881 huko Roma. Mapadre wa jimbo walikuwa wanachama wake wa kwanza. Theresa Von Wullenweber (kwa sasa Mwenye Heri Maria wa Mitume) alijitoa mwenyewe kwa Shirika hilo mwaka 1882. Idadi kubwa ya walei wa rika zote ilijiunga na Shirika hili.
3. Siku hizi Familia ya Wasalvatoriani ina matawi matatu yanayojitegemea: Shirika la Mungu Mwokozi, Shirika la Masista wa Mungu Mwokozi na Jumuiya ya Kimataifa ya Mungu Mwokozi. Tunaunganishwa kwa majitoleo yetu kwa utume uliokusudiwa na Mwanzilishi wetu, tukiunda familia moja
   ya mitume wenye bidii wanaotangaza kwa wote wokovu uliojionyesha katika Yesu Kristu (Tito 3:4). Kama azimio la asili la Padre Jordani lilivyokuwa kadri ya muda, wakati ujao kwa hakika utaleta watu wengine katika familia yetu kwa mwongozo wa Roho Mtakatifu.
4. Tunaishi wito wetu katika usawa na kukamilishana kadri ya hali na tofauti zetu za maisha, vipaji vyetu na tamaduni zetu.

MBILI
UTUME WETU

"…tangaza neno la Mungu, fanya bidii kila wakati,
karipia kwa uvumilivu wote na kufundisha .
Nenda, na kwa udumifu sema maneno yote ya uzima wa mlele kwa watu."
Padre Jordani: Kanuni. 1884

"Ndiyo, sisi sote tunatakiwa kujibidisha kujipatia zaidi na zaidi hii roho ya kitume."
Barua ya Mama Maria: 28 Juni 1900

5. Tukifuata nyayo za Mwokozi kama mitume, tumeitwa kuishi na kutangaza upendo wa Mungu usio na masharti,kuendeleza kazi ya Yesu ya kutoa maisha kwa kuleta wokovu kwa viumbe vyote na ukombozi kutoka kwa kila kitu kinachotishia utimilifu wa maisha. (Mt 28:19-20; Mk 16:15)
6. Mang'amzi yetu ya wokovu ya binafsi na ya jumuia ni mwendelezo na nguvu yetu kwa kutimiza utume wetu.
7. Tunakuza upendo wetu kwa Kanisa na kufanya kazi ndani yake kwa ufahamu wa kinabii kama mashahidi wa Injili. Tukiamini kwamba Padre Jordani na Mama Maria walikuwa na wito wa wabatizwa wote kuwa nguvu hai katika Kanisa na kwa ajili ya ulimwengu wa haki, tunaunda na kusaidia viongozi katika kazi ya uinjilishaji.
8. Roho yetu ya umataifa inaelezwa kwa njia na namna zote ambazo zinaongozwa na upendo wa Mungu.

    a. Tupo tayari kukabiliana na shida na changamoto za nyakati zetu za kihistoria, tukiruhusu alama za nyakati zitufumbulie njia na namna zitakazotumika.

    b. Tunawahusisha wengine katika utume wetu na kutafuta ushirikiano wa wale wanaohusika katika kuhamasisha ukweli, haki na kutetea uhai, kwa kuwapendelea zaidi fukara na wale ambao wananyanyasika katika utu na hadhi zao za kiutu.

    c. Tunafanya ukweli wa milele wa Neno wa Mungu na Imani yetu viwafikie watu wa tamaduni zote, rangi, jamii, tabaka za kijamii, taifa na dini.

    d. Tunaishi roho ya majadiliano katika mazingira ya tamaduni mbalimbali, dini mbalimbali na madhehebu mbalimbali.

9. Kila tawi la Kisalvatoriani linaeleza utume wetu wa pamoja kwa namna yake ya pekee.

TATU
MAISHA YETU KATIKA ROHO MTAKATIFU

"Ninajiweka mikononi mwako, Mwokozi na Mkombozi wangu. Pamoja Nawe, kwa ajili Yako, kwa njia Yako na ndani Yako, ninataka kuishi na kufa."
Padre Jordan: *Shajara ya Maisha ya Kiroho* I, 9: 15 Novemba 1875

"Ndiyo, tujibidishe kabisa kusali na kufanya kazi ili mapenzi ya Yesu, 'Ufalme wako ufike', yatimizwe."
Mama Maria: *Barua*, Mei 20, 1901

10. Tukiwa ndani ya ulimwengu halisi, chimbuko la maisha yetu ya kiroho ya mtu binafsi na kijumuiya li katika mang'amzi yetu juu ya Mungu Baba. Yesu kristu aliyekuja kutoa maisha kwa ajili ya wote, ndiye chemichemi na kiini cha maisha yetu ya kiroho, pamoja na Maria Mama yake, tunampeleka kwa wengine Mwokozi ambaye tumemjua wenyewe. Roho mtakatifu anatulinda na kutuangaza kwenye njia.
11. Tafakari yetu ya Neno la Mungu katika mwanga halisi wa hali yetu,na katika kuadhimisha Sakramenti, tunaunganisha sala zetu na matendo. Kwa kufanya hivyo tunajibidisha kuishi wito wetu wa Utakatifu na kuwahimiza wengine kufanya hivyo hivyo.
12. Ushuhuda wa Padre Jordani na Mama Maria unatuongoza kuwa watu wa sala, kuukumbatia kwa mapendo Msalaba kwa ajili ya utume wetu, kuwa na tumaini lisilotetereka katika Maongozi ya Mungu na kuishi maisha yasiyo na makuu, na kuwa na ibada ya pekee kwa Maria kama Mama wa Mwokozi.
13. Tunaonyesha wema na ukarimu wa Mungu katika hali zote mbili katika utume wetu na jinsi tunavyohusiana kama wanafamilia ya Kisalvatoriani. Katika sala na majadiliano, tanatafuta kumfahamu kila mmoja wetu na kuwa tayari kusameheana.

NNE
USHIRIKIANO WETU

"Zaidi ya yote, wanachama watakuza upendo ili waonekane kuwa washirika wa mitume, wakichukua kama urithi maneno ya mwalimu wetu mkuu, Yesu Kristu…, 'Amri mpya nawapeni, kwamba mpendane; kama nilivyowapenda ninyi, nanyi pia mpendane'."
Kanuni za Daraja la kwanza la Shirika Fundishi la Kitume, 1882.

14. Kama familia ya Kisalvatoriani, tunatoa ushuhuda wazi wa wanaume na wanawake kutoka tamaduni na mazingira mbalimbali tukifanya kazi bega kwa bega katika utume wetu. Tunakuza imani na heshima katika tofauti zetu, tukijifunza kutoka kwa wenzetu, na kuthamini mchango ambao kila mmoja anaweza kutoa kwa maisha na utume wetu.

15. Ingawa matawi matatu kila moja linajitawala, tunaonyesha ushirikiano wetu katika kuiishi karama yetu. Tunashirikiana katika mipango mipya ambayo vipaji vya wote vinahitajika, kwa kuyasaidia matawi mengine, pale inapowezekana, katika utume na shughuli zao.

16. Familia yote ya Kisalvatoriani inashiriki katika kazi ya kuhamasisha katika hali ya kufahamiana na kukua kwetu katika hali ya kujifahamu kwa kushiriki katika mikusanyiko, majadiliano na miradi ya pamoja.

17. Viongozi wetu wanaratibu uhusiano kati yetu na kutuhamasisha kuelewa utambulisho na umataifa wetu kama Familia ya Kisalvatoriani na kujituma kwetu katika mshikamano kati ya matawi matatu.

    a. Katika ngazi ya kitaifa katika nchi zenye wanachama wa matawi mawili au matatu ya Familia ya Kisalvatoriani, ushirikiano unahimizwa kwa njia ya bodi za uongozi wao na kwa njia ya uongozi wa pamoja wa kitaifa na kuunganisha pamoja wawakilishi kutoka katika kila tawi.

    b. Katika ngazi za kimataifa, ushirikiano unahimizwa kwa njia ya mikutano ya bodi ya uongozi wa kimataifa, kamati za pamoja na kwa mikutano mikuu ya mapadre/mabruda, masista pamoja na mikutano ya bodi ya uongozi wa Jumuiya ya Kimataifa ya Mungu Mwokozi katika kipindi cha mwaka uleule.

    c. Viongozi wa matawi yote matatu wanashirikiana katika kufanya maamuzi yanayogusa moja kwa moja familia yote ya kisalvatoriani.

HITIMISHO

Kama wafuasi wa Padre Francis Jordan na Mama Maria wa Mitume,na tukijazwa na roho yao ya Kimisionari, tunaipokea Katiba hii Kuu kama kielelezo cha utambulisho wetu kama Familia ya kisalvatoriani. Tunaomba kwa maombezi ya Baba Fransis na Mama Maria ili kila mmoja wetu apokee wito wetu wa Kisalvatoriani kwa ari na kwa shukrani.